Habarileo Ijumaa Oktoba 3, 2025 Pg 3

# Mabasi 90 yahudumia njia ya Kimara-Kivukoni

**Na Prisca Pances**

SERIKALI imesema imeamua kuingiza mabasi 60 mapya kwenye Barabara ya mabasi yaendayo haraka njia ya Kimara hadi Kivukoni mkoani Dar es Salaam.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amesema njia hiyo ilikuwa na mabasi 30 yanayofanya kazi, hivyo sasa njia hiyo itakuwa na mabasi 90.

Majaliwa alisema hayo alipofanya ziara kukagua hali ya utoaji huduma ya usafiri kwa mabasi yaendayo haraka kwa njia ya Kivukoni hadi Kimara.

"Serikali yenu baada ya kuruhusu makampuni binafsi, tumeona tuchukue mabasi 60 kutoka Kampuni ya Mofat yaingie katika barabara hii na yameanza kutoa huduma leo. Malengo yetu ni kuondoa kadhia ya usafiri kwenye njia hii" alisema.

Aliongeza: "Yatajumulishwa na haya 30 yaliyokuwa yakitoa huduma awali na leo mabasi mapya yameanza kutoa huduma na yatakuwa yanatumia umeme na gesi. Natoa wito kwa makampuni mbalimbali kujitokeza na kujenga vituo vya gesi."

Majaliwa ameiagiza kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (UDART) na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) wasimamie matumizi ya kadi za kielektroniki katika utozaji wa nauli, badala ya kutumia fedha taslimu ili kudhibiti upotevu wa mapato.

"Na tumeagiza kadi hizi zisiwe za mabasi haya peke yake, tunataka zitumike kwenye viwanja vya mipira, usafiri wa Azam marine, SGR (Reli ya Kisasa), vituo vya mabasi. Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Jerry Silaa, tunataka hili likamilike kwa haraka" alisema.

Aliongeza: "Waziri mwenye dhamana kwenye suala la teknolojia, hakikisha suala hili linakamilika kwa wakati na kadi hizi zitakapotoka, hakikisha zimeunganishwa na mifumo yote ili kadi moja mtu aweze kuitumia katika shughuli mbalimbali, ikiwemo kusafiri, kuangalia mpira na kufanya manunuzi."

Majaliwa amemuagiza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila na DART wasimamie usafiri huo, ili kupunguza kero ya usafiri wa mabasi hayo.

Majaliwa aliwataka wananchi kufuata utaratibu uliowekwa ili kuondoa hali ya kugombania magari, iliyosababisha uharibifu wa miundombinu hapo awali.

"Serikali imeamua kuruhusu sekta binafsi kushiriki kwenye biashara ya usafiri wa mwendokasi. Tayari makampuni manne yamesaini mikataba na kuanza kuagiza mabasi. Kampuni ya Mofat peke yake imekwishaingiza mabasi 150 kwa ajili ya njia za katikati ya jiji na Mbagala," alisema.

Majaliwa alisema mabasi mapya yamegawanywa kwenye njia tofauti, ikiwemo ya Kivukoni–Kimara, katikati ya jiji–Mbagala, Mbagala Rangi Tatu kupitia Kigamboni na Gongo la Mboto.

Alisema serikali imetangaza zabuni kwa kampuni binafsi kuwekeza katika vituo vya kuchaji magari ya umeme na gesi na kituo cha kwanza cha gesi kipo hatua za mwisho za ukamilishaji

Majaliwa alisema serikali inaendelea pia na ujenzi wa barabara za mwendoksasi za Morocco–Mwenge–Tegeta na Ubungo–Buguruni kuelekea Kiwanja cha Ndege cha cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), ili kupunguza msongamano.

Chalamila alisema kuongezwa kwa mabasi mapya ya mwendokasi kumetoa suluhisho la changamoto za usafiri Dar es Salaam na akaahidi miundombinu italindwa.

CamScanner

# Govt introduces 60 new buses on Kimara-Kivukoni BRT route

**By Guardian Reporter**

THE government has introduced 60 new buses to the Dar es Salaam Bus Rapid Transit (BRT) system, operating on the Kimara-Kivukoni route, which previously had only 30 active buses. The move aims to ease the shortage of vehicles that had been causing significant transport challenges for commuters.

The addition brings the total number of buses on the route to 90. Prime Minister Kassim Majaliwa made the announcement in Dar es Salaam yesterday during an inspection tour of the BRT operations along Kimara-Kivukoni corridor.

"After allowing private companies to join the system, your government decided to add 60 buses from Mofat Company to this route, and they have started operating today (yesterday). Our goal is to resolve the transport difficulties along this line," he said.

In a related directive, the PM ordered UDA Rapid Transit Public Limited Company (UDART) and Dar es Salaam Rapid Transit (DART) to enforce the exclusive use of electronic cards for fare payment instead of cash in order to curb revenue leakages.

"We have directed that these cards should not only be used on these buses but also in football stadiums, marine ferries, the SGR railway, and bus terminals. Minister for Information, Communication and Technology Jerry Silaa has been instructed to ensure this integration is completed quickly," he added.

Majaliwa further directed Dar es Salaam Regional Commissioner's Office and DART to strengthen oversight of the BRT service to ensure smooth operations and address commuter concerns.

He urged the public to trust the government's measures, assuring that the transport challenges in the city will be significantly reduced. "Let us have confidence that what has been happening is now behind us," he said.




**One of the newly deployed high-capacity commuter buses designed for fast, reliable and comfortable transit in Dar es Salaam in business on the Kimara to Posta-Kivukoni route yesterday. They are under the Dar es Salaam Bus Rapid Transit (BRT) system, itself operated by UDART.** Photo: Correspondent Imani Nathaniel

CamScanner

Ijumaa oktoba 3 2025

## Nukuu



Kupenda kushinda ni tabia. Bah
pia ni tabia.

*Vince Lombardi, Juni 11, 1913 -*

# Usafiri mwendokasi ukidhi mahitaji ya umma

Kero ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka (maarufu mwendokasi) jijini Dar es Salaam imefikia hatua ya kukatisha tamaa, hasa kwa wakazi wanaosafiri kutoka Mbezi hadi Gerezani au Kivukoni. Kwenye njia hiyo abiria hulazimika kukaa vituoni kwa muda mrefu huku wakigombea nafasi kwenye mabasi machache yanayopatikana.

Huduma iliyolenga kupunguza adha ya usafiri, sasa imegeuka chanzo cha msongamano, usumbufu na kuamsha vurugu miongoni mwa wananchi.

Hata hivyo, suluhisho ya pekee na uhakika ni kuhakikisha kuna mabasi ya kutosha yanayokidhi mahitaji halisi ya abiria kwa nyakati tofauti za asubuhi, mchana na jioni. Bila idadi ya kutosha ya mabasi, hakuna aina yoyote ya huduma bora inayoweza kutekelezwa kwa ufanisi na kuridhisha umma.

Huduma ya mwendokasi haitatengenezwa kwa ahadi pekee, lazima kuwe na mabasi ya kutosha, yaliyo katika hali nzuri na yanayoendeshwa kwa ratiba ya kueleweka.

Hakuna mantiki ya kuwa na vituo vilivyojengwa kwa mabilioni ya fedha, lakini abiria wasiwe na uhakika wa kuondoka hapo kwa wakati. Matatizo haya hayawezi kutatuliwa kwa kuleta mabasi machache kila baada ya miaka fulani bali yanahitaji mfumo wa uendeshaji unaojali mahitaji ya miji mikubwa na ongezeko la watu.

Mbaya zaidi, kwenye maeneo tajwa yenye shida, usafiri mwingine wa umma, hasa daladala, ulizuiwa mapema kupisha mabasi ya mwendokasi ambayo hayakufanya vizuri. Abiria wa maeneo hayo wanajikuta hawana chaguo jingine, bali kusubiri mabasi yasiyokuwapo au wengine kutegemea bajaji na bodaboda.

Tangu kuanza kwa huduma ya mwendokasi mwaka 2016, upungufu wa mabasi na uchakavu wa yaliyopo vimekuwa changamoto ya muda mrefu, kwa bahati mbaya haijawahi kutatuliwa kwa namna ya kudumu.

Ni muhimu Serikali itambue kuwa, huduma za usafiri si hisani kwa wananchi, bali ni haki yao ya msingi inayopaswa kupewa uzito mkubwa kama ilivyo elimu na afya.

Juzi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila amefanya ukaguzi kwenye baadhi ya vituo vya mabasi na kukiri hadharani kuwa, hali ya huduma ni mbaya, akieleza mabasi yanayofanya kazi kwa sasa hayafiki hata 40, licha ya mradi huo ulilenga kuwa na zaidi ya mabasi 300.

Ni jambo la kusikitisha kuona huduma hii ya usafiri iliyoonekana mkombozi kwa wakazi wa Dar es Salaam, imegeuka chanzo cha mateso kwao. Wananchi wanasukumana, wanagombania mabasi na wengine hulazimika kushushwa kwa nguvu kutoka ndani ya magari ili milango iweze kufungwa.


Hali hii ni aibu kwa mji mkuu wa biashara wa Dar es Salaam, unaotarajiwa kuwa mfano wa maendeleo ya miundombinu na huduma bora kwa wananchi wake.

Ni dhahiri hata haya mabasi yaliyoazimwa kwa mwendeshaji wa mradi wa Mbagala hayataweza kufua dafu, kinachotakiwa ni mwekezaji mpya mwenye mabasi ya kutosha. Zaidi ya hapo, ni lazima Serikali ijifunze kutokana na hali hii na kuweka mfumo wa kudumu wa usimamizi na ufuatiliaji wa huduma za usafiri mijini, huku ikikiri kwamba yenyewe imeshindwa kuendesha biashara hiyo, hivyo ikabidhi kwa sekta binafsi.

Mabasi kuharibika, kuchelewa au kutotosha si jambo la dharura wala ghafla, bali ni matokeo ya mifumo duni ya usimamizi na ukosefu wa ushindani katika utoaji wa huduma.

Katika hili, hatua ya kuingiza kuongeza mabasi ya kuazima na hata kubadili watendaji iwe kama mwanzo wa mabadiliko ya kweli na si suluhisho la muda mfupi.

## KING KINYA



**HUTOLEWA NA MWANANCHI COMMUNICATIONS LIMITED (MCL)**

MWANANCHI COMMUNICATIONS LTD

Barabara ya Mandela, SLP 19754, Dar es Salaam
+255 22 24 50875, 0754 780647, 0765 864917
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Rosalynn Mndolwa-Mworia:** Mkurugenzi Mtendaji
**Mpoki Thompson:** Mhariri Mtendaji Mkuu
**Joseph Damas:** Mhariri Mtendaji

*Tunawezesha taifa*

HUZUNI

# Samia, wadau uhifadhi wamlilia shujaa wa sokwe na mazingira

**Na Godfrey Mushi, ARUSHA**

WADAU wa sekta za utalii na uhifadhi nchini, wamemlilia nguli wa utafiti wa maisha ya sokwe mtu na mwanasayansi mashuhuri duniani wa utafiti na tabia za wanyama, Dk. Jane Goodall (91), aliyefariki dunia juzi nchini Marekani.

Dk. Goodall atakumbukwa kwa mambo mengi, ikiwamo kutoa mchango mkubwa nchini katika elimu ya viumbe na mwalimu muhimu wa uhifadhi, anayeaminika kuwa na ujuzi mpana na wa kina juu ya viumbe hao kuliko mtu mwingine yeyote.

Kwa mujibu wa Taasisi ya Dk. Jane Goodall, alifariki dunia juzi Marekani alipokwenda kutoa mhadhara.

Kutokana na kifo chake, Rais, Samia Suluhu Hassan katika ujumbe wake, ameeleza kusikitishwa na kitendo hicho cha rafiki huyo mkubwa wa Tanzania, mwana mazingira na mtafiti maarufu wa sokwe duniani.


Rais Samia ameandika katika ukurasa wake wa mtandao wa kijamii: "Kwa huzuni kubwa, nimepokea taarifa za kifo cha Dk. Jane Goodall, mtaalamu mashuhuri wa wanyamapori, mtafiti wa sokwe, mchunguzi na rafiki wa Tanzania.

"Amefanya kazi ya kipekee (Dk. Jane Goodall) katika Hifadhi ya Taifa ya Gombe, iliyobadilisha uhifadhi wa wanyamapori na kuiweka Tanzania katika ramani ya dunia ya jitihada za kimataifa za kulinda sokwe na mazingira. Urithi wake utaendelea kuishi."

Aidha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abbas, katika ukurasa wake ameandika kuwa kazi yake ya 'primatology' kule Gombe na Mahale, Kigoma, hakika itaendelea. Primatology, ni utafiti wa tabia, baiolojia, mageuzi na taksonomia ya nyani.

**TANAPA YAMLILIA**

Katika ukurasa wa mitandao ya kijamii wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Shirika hilo limeandika: "TANAPA inaheshimu maisha ya Dk. Jane Goodall ambaye mchango wake wa ajabu katika utafiti wa Sokwe huko Gombe na duniani kote, umeacha urithi wa kudumu unaohamasisha ubinadamu na uhifadhi wa maliasili duniani kote."



Dk. Jane Goodall

Wakati wa uhai wake, mwaka 2001 alianzisha Taasisi ya Tanzania ya Jane Goodall Tanzania (JGI-TZ). JGI Tanzania na washirika wake, tangu wakati huo imekuwa ikifanya utofauti kwa njia ya uhifadhi wa msingi wa jamii, miradi ya utafiti wa sokwe mtu, elimu ya vijana na matumizi ya sayansi na teknolojia.

Atakumbukwa kwa kufanya kazi kwa karibu na jumuiya za mitaa nchini Tanzania, kwa JGI Tanzania kutekeleza shughuli za utafiti wa wanyamapori katika Hifadhi ya Taifa ya Gombe kupitia Mpango wa Kituo cha Utafiti wa GOME (GSRC).

Shughuli za utafiti zilianza nyuma ya 1960 wakati Dk. Jane Goodall alipowasili Gombe Julai 14, 1960.

Ndiye aliyefanya utafiti wa sokwe mtu ukapanuka nje ya hifadhi ya misitu ya vijiji na hifadhi ya misitu ya mitaa, inayomilikiwa na kusimamiwa na halmashauri za wilaya za Uvinza mkoani Kigoma na Tanganyika katika mkoa wa Katavi.

Kwa zaidi ya nusu karne, Dk. Goodall alijulikana kwa utafiti wake wa kina kuhusu sokwe mtu na alibadilisha mtazamo wa dunia juu ya tabia na hisia za wanyama.

Utafiti wake mbalimbali ulithibitisha kwamba sokwe wanaonesha hisia na tabia zenye kufanana kwa karibu na za binadamu, jambo lililovunja mipaka ya kisayansi na kijinsia.

"Ugunduzi wa Dk. Goodall kama mtaalamu wa ethologia ulileta mageuzi katika sayansi na alijitolea bila kuchoka kulinda na kurejesha mazingira yetu ya asili," ilisema taarifa ya taasisi hiyo kupitia mitandao ya kijamii.

Safari ya Goodall ilianza mwaka 1960 alipowasili katika Hifadhi ya Sokwe ya Gombe Stream Tanzania, kwa mwaliko wa mtaalamu maarufu wa akiolojia na anthropolojia, Dk. Louis Leakey.

Wakati huo, akiwa na umri wa miaka 26 na bila elimu ya juu rasmi, alianzisha utafiti uliokuwa wa kipekee duniani kwa kuchunguza sokwe katika makazi yao ya asili.

Awali, sokwe walimkimbia kwa hofu. "Walikuwa hawajawahi kuona nyani mweupe (mtu mzungu) kabla," alisema Dk. Goodall katika mahojiano na Deepak Chopra mwaka 2019.

Mbali na utafiti wake, Dk. Goodall alitambulika kimataifa kwa mchango mkubwa wa kutetea uhifadhi wa mazingira.

Alitunukiwa heshima ya Dame of the British Empire mwaka 2004, akapewa Tuzo ya Heshima ya Uhuru wa Rais wa Marekani (Presidential Medal of Freedom) mwaka 2025 na mwaka 2002 aliteuliwa kuwa Balozi wa Amani wa Umoja wa Mataifa.

Umoja wa Mataifa kupitia ukurasa wake wa X (zamani Twitter) ulisema: "Goodall alifanya kazi bila kuchoka kwa ajili ya sayari yetu na viumbe wake wote, akituachia urithi wa kipekee kwa binadamu na mazingira."

Kazi na maisha yake pia vilioneshwa kwenye filamu na vipindi vya televisheni, kikiwamo kipindi maalum cha 'Miss Goodall and the World of Chimpanzees' kilichorushwa na CBS mwaka 1965 kikiwa kimenakili maisha yake Gombe, Tanzania.

Goodall ataendelea kukumbukwa kama mwanamke shujaa, mtafiti na mtetezi wa mazingira aliyeacha alama isiyofutika katika historia ya sayansi na dunia kwa ujumla.

**2001**
**alianzisha Taasisi ya Tanzania ya Jane Goodall Tanzania (JGI-TZ). JGI Tanzania na washirika wake, tangu wakati huo imekuwa ikifanya utofauti kwa njia ya uhifadhi wa msingi wa jamii, miradi ya utafiti wa sokwe mtu, elimu ya vijana na matumizi ya sayansi na teknolojia.**

The Guardian

## JOB VACANCY

## SUPPLEMENT EDITOR

***The Guardian Limited***, publishers of Tanzania's leading daily newspapers, The Guardian and Nipashe, is seeking to recruit a Supplement Editor to join the team.

The Supplement Editor will be responsible for planning, writing, and editing high-quality advertorials and special supplements that meet both editorial standards and client expectations.

**Key Responsibilities**
- Develop editorial plans for special supplements and advertorial features.
- Write, edit, and proofread content tailored to client needs while maintaining journalistic quality.
- Coordinate with advertisers, designers, and the editorial team to deliver timely, engaging content.
- Ensure accuracy, clarity, and creativity in all supplement publications.
- Manage multiple projects under tight deadlines.

**Qualifications & Experience**
- Bachelor's degree in Journalism, Mass Communication, or related field.
- Minimum 3 years' proven experience in editorial writing, editing, or content development.
- Strong writing and editing skills in English (Swahili is an added advantage).
- Experience in advertorials, marketing content, or corporate communication.
- Ability to work under pressure and meet deadlines.
- Excellent interpersonal and communication skills.

**Mode of Application**
Interested candidates should send their CV and cover letter to **vacancy@guardian.co.tz** before **6th October 2025**, Please remember to include the region you intend to work from in the subject/title of your application letter.

***NB: Only shortlisted candidates will be contacted.***

187090

**The Guardian Limited is an equal opportunity employer.**